**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

***Dodoma***
***14 Juni, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa wito kwa wananchi wa maeneo yanayozungukwa na Barabara ya Mzunguko wa Nje *(Outer Ring Road)* ya Jijini Dodoma kutumia fursa za miundombinu hiyo katika kuongeza uzalishaji wa kilimo na uongezaji thamani wa mazao kwa maendeleo yao na Taifa kwa ujumla.

Ametoa wito huo leo wakati akizungumza na wananchi katika eneo la Nala mara baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa barabara hiyo pamoja na mradi wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato.

Rais Dkt. Samia amesema kukamilika kwa miradi hiyo miwili mikubwa kutarahisisha usafirishaji wa mazao, pembejeo na bidhaa nyingine kwa gharama nafuu na kasi kubwa, hivyo ni jukumu la wananchi kujiandaa kuitumia kikamilifu kwa kuweka mipango madhubuti ya kuendeleza kilimo cha kisasa, hasa cha zabibu na alizeti ili kuongeza tija na kipato.

Aidha, Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa Serikali iliamua kuanzisha ujenzi wa Barabara ya Mzunguko wa Nje ya Dodoma yenye urefu wa kilomita 112.3 ili kukabili changamoto ya msongamano wa magari Jijini Dodoma na kurahisisha biashara na usafirishaji kutoka Dar es Salaam kuelekea Kanda ya Ziwa na nchi jirani.

Akizungumzia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Rais Dkt. Samia amesema uwanja huo utakuwa lango jipya la kimataifa litakalosaidia kukuza biashara, utalii na nafasi ya Dodoma kama makao makuu ya nchi.

Katika hotuba yake, Rais Dkt. Samia pia ametoa shukrani maalum kwa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Akinwumi Adesina, kwa ushirikiano na ufadhili

uliotolewa na AfDB kwa miradi mbalimbali ya barabara nchini, ikiwemo ya Barabara ya Kabingo–Kasulu–Manyovu, Dodoma–Babati, Mnivata–Masasi, Sakina–Tengeru, ufadhili kwa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania, pamoja na vipande viwili vya reli ya kisasa (SGR) inayounganisha Tanzania na nchi jirani za Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Akizungumzia kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo, Rais Dkt. Samia amezielekeza Wizara za Ujenzi na Uchukuzi kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati kama ilivyopangwa na kwa ubora unaotakiwa, huku akisisitiza umuhimu wa kuitunza ipasavyo ili idumu kwa muda mrefu na kutoa tija iliyokusudiwa kwa Taifa.

Katika kutambua mchango mkubwa wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika katika utekelezaji wa miradi hiyo na katika kuchangia maendeleo ya miundombinu nchini Tanzania, Rais Dkt. Samia ameridhia pendekezo la Wizara ya Ujenzi la kuipa jina barabara hiyo ya mzunguko wa nje wa Dodoma la "Barabara ya Dkt. Akinwumi Adesina."

Akiwa nchini, Dkt. Adesina alitunukiwa Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Sayansi (Honoris Causa) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutokana na mchango wake mkubwa kwa maendeleo ya Bara la Afrika kupitia sera za fedha na programu bunifu za maendeleo.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu